**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA AFYA**

# UFAFANUZI WA MHE. UMMY ALLY MWALIMU (MB), WAZIRI WA AFYA WAKATI WA MKUTANO NA VYOMBO VYA HABARI KUHUSU HALI YA MFUKO WA TAIFA WA BIMA YA AFYA (NHIF) JIJINI DODOMA TAREHE 01 SEPTEMBA, 2022.

Awali ya yote, napenda kuchukua fursa hii kuvishukuru vyombo vya Habari na waandishi wote wa habari kwa kuendelea kushirikiana na Serikali katika kuhabarisha Umma kuhusu juhudi mbalimbali zinazofanywa na Serikali hususani katika kuimarisha upatikanaji wa huduma bora za afya kwa wananchi.

Kama mnavyofahamu, Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaendelea kuweka mazingira mazuri kwa wananchi wote kuwa na uhakika wa kupata huduma bora za afya karibu na maeneo yao kutokana na uwekezaji mkubwa unaofanywa wa ujenzi wa miundombinu ya utoaji wa huduma za afya ikiwemo Zahanati, Vituo vya Afya, Hospitali za Wilaya na Mikoa katika maeneo mbalimbali nchini sambamba na ununuzi wa vifaatiba vya kisasa, kuongeza bajeti ya dawa na vitendanishi na kuongeza ajira kwa watumishi katika Sekta ya Afya katika ngazi zote.

**Ndugu Wanahabari,**

Pamoja na jitihada zinazofanywa na Serikali katika kuimarisha huduma za afya, bado kuna changamoto ya kuongezeka kwa idadi kubwa ya wananchi

wenye magonjwa yasiyo ya kuambukizwa ambayo gharama zake ni kubwa. Kama mnakumbuka tarehe 29/08/2022 wakati nikifungua Mkutano wa Shirika la Afya Duniani (WHO) Kanda ya Afrika kuhusu Ugonjwa wa Kipindupindu jijini Dar es Salaam, niliweka msisitizo wa kuweka nguvu na jitihada katika kuzuia magonjwa badala ya kusubiri kutibu. Katika muktadha huo nilitoa angalizo kuwa hivi sasa nchini kwetu tunashudia ongezeko kubwa la magonjwa yasiyo ya kuambukiza ambayo matibabu yake ni gharama kubwa na hivyo kama tutachelewa kuchukua hatua stahiki katika kudhibiti magonjwa hayo, basi kuna hatari pia kwa Mfuko wetu wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) kuelemewa na gharama za matibabu kutokana na kuongezeka kwa idadi ya wanufaika wenye magonjwa yasiyoambukizwa na gharama zake, hali inayoweza kuathiri uhai na uendelevu wa Mfuko.

Kulingana na takwimu zilizopo, gharama za magonjwa yasiyo ya kuambukizwa zimeongezeka kutoka **shilingi bilioni 35.65** mwaka 2016/17 hadi **shilingi bilioni 99.09** mwaka 2021/22. Mathalani:

- Gharama za kuhudumia wagonjwa wa **saratani** wanaopata tiba za mionzi na chemotherapia (chemotherapy services), kupitia Mfuko ziliongezeka kutoka **shilingi bilioni 9 mwaka 2015/16** hadi kufikia **shilingi bilioni 22.5 mwaka 2021/22.**

- Kwa upande wa **huduma za matibabu ya figo** kwa wanachama wanaopata huduma ya kuchuja damu (hemodialysis services), gharama ziliongezeka kutoka **shilingi bilioni 9.5 mwaka 2015/16** kufikia **shilingi bilioni 35.44 mwaka 2021/22**. Pia idadi ya wagonjwa hawa wa figo imeongezeka **kutoka 280** mwaka 2014/15 hadi kufikia 2,099 mwaka 2021/22.

- Gharama za **matibabu ya moyo** kwa wanachama wa Mfuko wanaopata matibabu ya upasuaji wa moyo (minimal and invasive cardiac procedures), ziliongezeka kutoka **shilingi bilioni 0.5 mwaka 2015/16** hadi kufikia **shilingi bilioni 4.33 mwaka 2021/22**.

- Gharama za vipimo vya **CT scan na MRI** ziliongezeka kutoka **shilingi bilioni 5.43 mwaka 2015/16** hadi kufikia **shilingi bilioni 10.87 mwaka 2021/22**.

Kwa muelekeo wa takwimu hizi, ni wazi kuwa kama hatutachukua hatua madhubuti kama nchi, kuna uwezekano wa Mfuko kwa siku za mbeleni kushindwa kutimiza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria. Hatua hizo zinaanzia katika ngazi ya mtu mmoja mmoja kwa kubadili mtindo wa maisha kwa kuzingatia aina za vyakula tunavyokula, kuepuka uvutaji wa sigara na kufanya mazoezi nk. Kwa upande mwingine, Serikali kuendelea kubuni mikakati ya kukinga magonjwa haya na pia kupambana nayo kadri yanavyojitokeza.

***Ndugu Wanahabari,***
Pamoja na uwepo wa ongezeko kubwa la magonjwa yasiyo ya kuambukiza, sababu nyingine inayohatarisha uhai na uendelevu wa Mfuko huu ni vitendo vya udanganyifu vinavyofanywa na baadhi ya watoa huduma na wanachama wa Mfuko, vitendo hivi vinalenga kujipatia manufaa kinyume na utaratibu. Mathalani katika mwaka wa fedha 2021/22 jumla ya wataaluma 65 wamefikishwa katika mabaraza yao kutokana na kukiuka taratibu na miongozo ya taaluma za afya. Nimeieleza NHIF kuimarisha mikakati yake ya kupambana na vitendo vya udanganyifu pamoja na kuimarisha matumizi ya Mifumo ya TEHAMA.

Vilevile, changamoto nyingine iliyopo ni uwepo wa kundi kubwa la wananchi wanaojiunga na NHIF kwa hiari ambao, takribani asilimia 99 ni wagonjwa. Hatua hii imetokana na kutokuwepo kwa Sheria ya ulazima kwa wananchi kujiunga na Bima ya Afya. Kama mnavyokumbuka Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), ulianzishwa mwaka 2001 ukiwa umelenga kuwahudumia watumishi wa umma pekee. Lakini kutokana na uhitaji wa huduma hizi kwa wananchi wote, marekebisho ya Sheria yamekuwa yakifanyika mara kwa mara na kuruhusu makundi mbalimbali kuhudumiwa na Mfuko. Makundi haya ni kutoka katika Sekta rasmi binafsi pamoja na ile isiyo rasmi ambapo hadi kufikia mwezi Juni 2022, Mfuko unahudumia

takribani **wanufaika milioni 4.8** ikilinganishwa na **wanufaika 691,173** waliokuwa wakihudumiwa mwaka 2001/02. Hivyo uwepo wa takribani asilimia 99 ya wanachama waliojiunga kwa hiari ambao ni wagonjwa imekuwa ikiongeza gharama za matibabu zinazolipwa na Mfuko.

**Ndugu Wanahabari,**
Ni wazi kuwa hali ya ustahimilivu na uendelevu wa Mfuko ipo mashakani endapo hatua stahiki hazitachukuliwa. Hatua hizo ni pamoja na ;-

1. kuimarisha afua za kushughulikia magonjwa yasiyo ya kuambukiza katika hatua za awali ikiwemo kuyatambua mapema kabla ya kuwa na athari kubwa.
2. kuongeza idadi ya wanachama
3. kudhibiti vitendo vya udanganyifu vinavyofanywa na baadhi ya watoa huduma za afya
4. kudhibiti matumizi ya huduma yasiyo na tija
5. kupunguza gharama za matibabu nchini
6. kuwa na Mfumo endelevu wa kuhakikisha Mfuko unakuwa na fedha wakati wote kutoka katika vyanzo vyake vya mapato na katika hatua hii tunaishukuru serikali kwa kuwasilisha michango ya watumishi kwa wakati.

**Ndugu Wanahabari,**
Niwatoe wasiwasi wadau wa NHIF wakiwemo wanachama, watoa huduma pamoja na watanzania wote kuwa Serikali inaendelea kuchukua hatua stahiki kuhakikisha kuwa Mfuko huu unakuwa imara, endelevu na stahimilivu kwani kwa sasa, ni moja kati ya mfumo unaotumika katika kuhakikisha huduma za afya zinatolewa nchini. Mfuko huu ndio umekuwa tegemeo la watanzania wengi hususani wa kipato cha chini. Na Mfuko huu pia ndio umekuwa tegemeo la vituo vya kutoa huduma za afya nchini. Pamoja na kuwa na wanachama asilimia nane (8) tu ya Watanzania wote, vituo vingi vya kutolea huduma vinategemea mapato kutoka katika Mfuko kwa zaidi ya asilimia 70.

Katika kuhakikisha kuwa maamuzi yote yahusuyo Mfuko huu yanazingatia taratibu na miongozo ya kuendesha chombo hiki, tumefanya tathmini ya uhai na uendelevu wa mfuko kwa mujibu wa sheria na, hivyo tunatambua ni yapi yanapaswa kufanyika ili kuhakikisha mfuko wetu unakuwa endelevu na imara zaidi.  Matokeo ya awali yanaonesha uendelevu wa Mfuko huu unategemea sana ongezeko la wanachama watakaoandikishwa katika Mfuko huu. Serikali ipo katika hatua za mwisho za kuwasilisha Bungeni Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote ambayo itaweka mazingira kwa kila mtanzania kuwa na bima ya afya ili kuwezesha dhana ya kuchangiana gharama za matibabu na hivyo kuwaepusha wananchi katika hatari ya janga la umaskini pindi wakiwa wagonjwa au wanapougua. Uzoefu kutoka katika nchi nyingine unaonesha kuwa, kadri idadi ya wanachama inavyokuwa kubwa katika Mifuko hii ya bima za afya za umma kama NHIF, ndipo uwezo wake katika kugharamia matibabu unaongezeka na hivyo kuwa stahimilivu na endelevu kwa muda mrefu.

**Ndugu Wanahabari,**

Nimalizie kwa kurudia kuwatoa hofu wanachama  wa NHIF na wananchi kwa ujumla kuwa Serikali inaendelea kuchukua hatua za kuuimarisha Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ili kuwa endelevu na kuwanufaisha wananchi walio wengi zaidi. Hatutakubali kuona Mfuko huu unatetereka kwa sababu Changamoto zilizoko tunazifahamu na mikakati ya kuzishughulikia imeanza kutekelezwa.

**Asanteni sana kwa kunisikiliza.**

.